# e-GA yajivunia mafanikio miaka 10 ya mfumo wa baruapepe wa serikali

## >>WADAU wafurahishwa na uhakika wa mawasiliano salama serikalini

**Na MWANDISHI WETU**

ILIANZA kama wazo, kisha wataalamu wakaketi na kutengeneza Mfumo wa Baruapepe wa Serikali (Government Mailing System - GMS), ambao hivi sasa umetimia muongo mmoja wa mafanikio ya matumizi ya mfumo huu.

Kwa nini tusijenge mfumo wa baruapepe wa serikali, kila mtumishi wa umma afanye mawasiliano ya kiofisi kupitia mfumo huu?

Hili ndilo swali lililoifanya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kusanifu na kujenga mfumo wa GMS mwaka 2014, (wakati huo ikiitwa Wakala wa Serikali Mtandao – eGA).

Dhamira kubwa ya ujenzi wa mfumo huo ni kurahisisha mawasiliano kati ya taasisi za umma na wadau wake, sanjari na kuimarisha usalama wa taarifa za serikali katika karne hii ya sayansi na teknolojia, ambapo Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ni nyenzo muhimu na wezeshi katika utendaji kazi wa shughuli mbalimbali, zikiwemo za kijamii, kiuchumi na utoaji wa huduma kwa umma.

Itakumbukwa kuwa, kabla ya maendeleo ya sayansi na teknolojia, mawasiliano rasmi ya kiofisi baina ya taasisi na wadau wake yalikuwa yanafanyika kwa njia ya barua kwa kutumia makaratasi.

Njia hii ilikuwa na gharama kubwa na kuchukua muda mrefu, hivyo kupunguza tija na ufanisi katika utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa umma.

Katika jitihada za kutafuta suluhisho la changamoto hizo na kutokana na fursa ya maendeleo ya teknolojia, e-GA iliamua kusanifu na kuanza ujenzi wa mfumo wa Buruapepe serikalini (GMS) mwaka 2014.

Lengo la hatua hiyo ilikuwa ni kuboresha huduma ya mawasiliano baina ya taasisi za umma na wadau wake.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Mhandisi Benedict Ndomba, alisema mfumo wa GMS umerahisisha mawasiliano katika taasisi za umma na wadau wake mbalimbali na kuwawezesha viongozi na watendaji kufanya uamuzi kwa wakati.

Alifafanua kuwa, kabla ya kuwepo kwa mfumo huu, baadhi ya taasisi za serikali zilikuwa zinatumia mifumo ya baruapepe binafsi iliyotengenezwa na wakandarasi au kutumia mifumo ya baruapepe za muda mfupi kutoka kwa watoa huduma kama vile Yahoo na Gmail kubadilishana taarifa na nyaraka mbalimbali za serikali.

"Mifumo ya baruapepe ya aina hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali za kiusalama, kwani utunzwaji wa taarifa hizo haukuwa wazi kwa serikali kwa kuwa hakukuwa na makubaliano kuhusu usalama wa taarifa kati ya serikali na watoa huduma wanaomiliki mifumo hiyo," alisema.

Mhandisi Ndomba alibainisha kuwa, gharama za ununuzi na uendeshaji wa mifumo hiyo ya baruapepe zilikuwa kubwa na ufanisi wake ulikuwa mdogo, lakini hivi sasa matumizi ya mfumo wa GMS siyo tu umeokoa kiasi kikubwa cha fedha kwa serikali, bali pia umehakikisha usalama wa taarifa za serikali na uhakika wa upatikanaji wa huduma ya mawasiliano kwa njia ya baruapepe katika taasisi za umma.

Katika kipindi cha miaka 10 tangu kuanza kutumika kwa mfumo wa GMS, mawasiliano kwa njia ya baruapepe katika taasisi za umma yamekuwa ya uhakika na salama zaidi, ikiwa ni pamoja na kuziwezesha taasisi zote za umma kufanya mawasiliano kwa njia ya baruapepe kwa kutumia kikoa (Domain) cha ofisi husika hali inayowezesha utambulisho wa taasisi husika.

"Moja ya majukumu ya Mamlaka ni kutengeneza miundombinu na mifumo shirikishi kwa matumizi ya taasisi za umma kwa lengo la kupunguza urudufu wa mifumo ya TEHAMA.

Hivyo, usanifu, ujenzi na matumizi ya mfumo huu wa GMS, ambao sasa unatumiwa na taasisi zote za serikali, umeondoa utitiri wa mifumo ya baruapepe iliyokuwa ikitumiwa katika taasisi mbalimbali za umma, kupunguza gharama za uendeshaji kwa serikali kwa kila taasisi kununua na kuendesha mfumo wake wa baruapepe," alisema.

Alieleza hadi hivi sasa jumla ya taasisi na vituo vya kutolea



MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Mhandisi Benedict Ndomba

huduma zaidi ya 700 zinatumia mfumo wa GMS zikiwemo wizara na idara zinazojitegemea, mashirika ya umma, taasisi za umma, majiji, manispaa, mamlaka na wakala za serikali na halmashauri za wilaya.

"Mfumo wa GMS huboreshwa mara kwa mara kadri mabadiliko ya teknolojia yanavyojitokeza, kudhibiti usalama wa mfumo pamoja na kukidhi mahitaji ya watumiaji kwa kuwa, kadri mabadiliko ya teknolojia yanavyojitokeza. Pia mahitaji ya watumiaji katika mfumo huongezeka na wakati mwingine inatupasa kuongeza 'features'mpya kukidhi mahitaji ya watumiaji," alisema.

Pia, kuwepo kwa mfumo wa baruapepe wa serikali kumewezesha taasisi zote za umma kuwa na baruapepe zenye kikoa cha jina la taasisi husika kwa watumishi wake wote bila kujali taasisi ina uwezo kifedha au la.

### FAIDA ZA MFUMO WA GMS

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Wahasibu Tanzania (NBAA), Pius Maneno alisema mfumo wa GMS umerahisisha utumaji na upokeaji wa barua ndani ya taasisi za umma kwa kuwa, awali utumaji wa barua za kawaida ulikuwa unatumia muda mrefu hadi kufika ofisi iliyokusudiwa na muda mwingine barua hiyo hufika kwa kuchelewa na kuathiri utekelezaji shughuli za taasisi.

"Hivi sasa kupitia GMS kila taasisi imetengenezewa akaunti maalumu ya kutuma barua. Hapa NBAA tunatumia barua@nbaa.go.tzna baada tu ya kubonyeza kitufe cha kutuma, barua hiyo inakuwa imefika sehemu husika bila kuchelewa," alisema Maneno.

Ofisa TEHAMA Mwandamizi kutoka Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Salumu Ally Kulindwa, aliipongeza e-GA kwa kutimiza miaka 10 ya matumizi ya mfumo wa Baruapepe Serikalini (GMS) na kuishauri uimarisha ushirikiano zaidi kati yake na taasisi nyingine za umma ikiwemo COSTECH.

"Katika miaka 10 ya matumizi ya mfumo wa GMS, sisi COSTECH tunajivunia mfumo huu kwani e-GA imekuwa ikitoa ushirikiano wa haraka pale tunapopata changamoto yoyote katika matumizi ya mfumo huu au hata mfumo mwingine.e-GA hutatua changamoto hizo na kutoa mrejesho kwa wakati," alisema.

Aliongeza kuwa, COSTECH imekuwa ikipata ushauri kutoka e-GA wa masuala mbalimbali ya TEHAMA, hivyo ushirikiano huo umekuwa chachu katika kuimarisha matumizi ya TEHAMA na ujenzi wa Serikali Mtandao.

Ofisa Uhusiano na Mawasiliano Mwandamizi wa Bodi ya Wahasibu Tanzania (NBAA), Magreth Kageya alieleza kuwa, mfumo wa GMS umerahisisha utumaji na upokeaji wa taarifa za serikali kwa taasisi za umma, kwa kuwa taarifa hizo zinapita mahali salama.

Aliongeza hata mpokeaji wa taarifa anakuwa na uhakika anapokea taarifa kutoka sehemu husika kwa kuwa baruapepe zote zinakuja na jina la mtumaji, taasisi pamoja na kikoa cha go.tz.

"Hivi sasa usiri na usalama wa taarifa za serikali umeongezeka, mtumishi anapotuma taarifa mbalimbali zinazohusu serikali anapata uhakika kuwa taarifa au nyaraka zinapotumwa zinakuwa ni salama na hazitoki nje ya Tanzania, hivyo kudumisha usiri wa taarifa hizo na kulinda maslahi ya taifa letu," alisema.

Ofisa Utumishi Mkuu kutoka Idara ya Utawala na Rasilimali Watu Bohari Kuu ya Dawa (MSD), Dk. Adolar Beatus Duwe, alisema awali gharama za uendeshaji wa mifumo ya baruapepe katika taasisi za umma zilikuwa kubwa na ikitokea changamoto yoyote ya mfumo ilibidi kumlipa mkandarasi alete mtaalamu aliyejenga mfumo huo atatue changamoto husika.

Mkurugenzi wa Usimamizi wa Huduma za TEHAMA wa e-GA, Ricco Boma alieleza a kuwa, katika kuhakikisha mfumo wa GMS umehuishwa kutoka GMS tolea la kwanza (GMS 1.0.0) hadi GMS toleo la nne (GMS 4.0.0) kutokana na kupitia hatua mbalimbali za uboreshwaji, ikiwemo kuunganishwa na mifumo mingine ya TEHAMA kama viule mfumo wa Ofisi Mtandao (e-Office), Mfumo wa Uendeshaji wa Shughuli za Taasisi (ERMS) na Mfumo wa Ununuzi (NeST).

Kuhusu kuwajengea uwezo maafisa wanaotumia mfumo wa GMS, Mkurugenzi huyo alisema Mamlaka inatoa mafunzo mbalimbali ya usimamizi wa mfumo huo, ikiwa ni njia mojawapo ya kuwajengea uwezo maofisa wa vitengo vya TEHAMA serikalini wasimamie ipasavyo uendeshaji wa mfumo huo kwa ufanisi zaidi.

Meneja wa Huduma za Sheria wa e-GA, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Polisi (SACP) Rafael Rutahiwa, alitoa rai kwa watumishi wote wa taasisi za umma, kutumia mfumo wa GMS, kila wanapofanya mawasiliano ya serikali kwani kutokufanya hivyo ni uvunjifu wa Sheria ya Serikali Mtandao ya Namba 10 ya Mwaka 2019.

SACP Rutahiwa aliwataka watumishi wote wanaotumia mfumo wa GMS kuwasilisha changamoto wanazokutana nazo kwa maofisa TEHAMA wa taasisi husika ziwasilishwe katika Dawati la Msaada wa Kiufundi kupitia Mfumo wa Huduma kwa Wateja, ambao unapatikana kupitia kiungo cha https://helpdesk.ega.go.tz saa 24 siku saba za wiki kwa mwaka (24/7/365) au kwa kupiga simu namba 0764292299 au 0763292299, ambapo zitafanyiwa kazi kisha kutoa mrejesho kwa muhusika.

Katika kuadhimisha miaka 10 ya matumizi ya Mfumo wa Baruapepe wa Serikali (GMS) ni wazi kuwa faida nyingi zimepatikana kama zilivyobainishwa, ambapo miongoni mwao ni kuongezaka kwa tija na ufanisi wa huduma ya mawasiliano serikalini na kuimarika kwa usalama wa taarifa za serikali.

CamScanner